

MATUMAINI PROG NO:2422

TITLE: TEST FOR CHRISTIANS

SUMMERY: KINATUHIMIZA KUHUSIANA NA NJIA ZA KUFANYIKIA KUWA MRISTO WA KWELI.

TEXT: WAEBRANIA 13:1-9.

MADA: MTIHANI KWA WAKRISTO.

.....

Hebu kwanza kabisa tukapate kuomba kabla ya kuendelea na somo hili la leo.
Natuombe;

OMBI.... Jehovah Rafa,Jehovah Nissi, Jehovah Jireh; tunakushukuru kwa sababu ya ulinzi na zaidi mno uwepo wako. Tunapolianza somo hili la leo kuhusiana na mtiani wetu kama Wakristo ili kufanyika kuwa wano. Fungua mioyo yetu ili tukaweze kulielewa vyema. Ni kwa Yesu tumeomba, Amina.

Msikilizaji wangu mpendwa,,, ni fursa nyingine ya kufurahia maana Mungu wetu ametujalia tena nafasi ya kujifunza kutoka Nenoni mwake. Ni tumaini langu kwamba unaendelea vyema. Karibu tuanze somo letu la leo lenye kichwa,,,*mtihani kwa Wakristo.*

Kumbuka tu ya kwamba malengo yangu ya kupatana nawe kuptia kwenye idhaa hii ,, bila shaka ni kufundishana kulihusu neno lake Mwenyezi Mungu.

Kipindi hiki ni cha Matumaini kutoka TWR Kenya.

Somo ni kutoka kwenye Waebrania 12:25-29.

Pale mwisoni mwa fundisho leo,, nitakuwa na kupatia anwani yangu ya mawasiliano kati yangu nawe.

Nataka kwanza kabisa ukabarikiwe kupitia kwa wimbo huu

WIMBO:

Ni kweli kabisa ya kwamba maisha ni safari ndefu yenye vikwazo na majaribu lakini kwa imani tutashinda tu. Asante sana mtumishi **Happy Mlinga** kwa wimbo huo kwa jina **tutashinda**

Mimi naitwa, Vincent Amara.

Msilizaji wangu,,,Katika kitabu cha Waraka 1 Wakorintho 13:4-5 , tunaweza kuyapata maelezo fuatayo ambayo ni ya Kimungu. Maelezo haya ni; “Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo haujivuni.

Swali langu kuu kwako kama Mkristo ni..Je, mapenzi yako yanalingana na maelezo haya ambayo nimeweza kuyataja hapo juu?

Mimi kwa upande wangu,,,nataka ukweli huo uusafishe upendo wangu. Ninayo imani ya kuwa,,,hata nawe,,,kwa upande wako,, unaweza kufanya vivyo hivyo.

Rafiki yangu,,,nataka kukufichulia hili,,,,.Sisi hapa mara kwa mara,hupata barua kutoka kwa msikilizaji anayeyatokeza maswali haya,, katika barua yake.

Kwanza kabisa ni je,“Mkristo ni nani? Pili ni kuwa,,,Je,,Ukristo ni nini?

Naam, mimi ni Mkristo,,, na ninajua ya kwamba kunao Wakristo wengine wengi humu ulimwenguni.

Lakini sote lazima tukubali kushindwa maana sisi hukosea kila wakati.

Ndugu yangu,,licha ya kuyafanya makosa,,,jambo hilo haliwezi kuubadilisha ukweli kwa njia yoyote maana,,,katika mambo mengi,,ukweli hujidhihirisha na zaidi mno kuimarika.

Kunao Wakristo wa kweli na ninaamini Mungu anaweza kukufanya kuwa mmoja wao. Biblia hutufunulia sifa ambazo Wakristo wa kweli wanapaswa kuwa nazo. Sisi kama Wakristo tunaweza kuzijaribu tabia hizo bila shaka.

Mtu wangu,,,Majaribu matatu kwa Wakristo yanapatikana katika Waraka huu kwa Waebrania 13:1-9.

Neno linasema hivi;

1. Upendo wa kindugu uendelee.

2. Msisahau kuwakaribisha wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua.
3. Wakumbukeni waliofungwa kana kwamba mmefungwa pamoja nao; na wale wanaodhulumiwa, kama ninyi nanyi mlivyo katika mwili.
4. Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; bali waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.
5. Mazungumzo yenu yasiwe na choyo; muwe radhi na vitu mlivyo navyo;
6. Tuseme kwa ujasiri, Bwana ndiye msaidizi wangu, sitaogopa mwanadamu atanitenda nini.
7. Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu, ambao kwa kuuchunguza mwisho wa mwenendo wao, muige imani yao.
8. Yesu Kristo ni yeye yule jana na leo na hata milele.
9. Msichukuliwe huku na huku na mafundisho mengine ya kigeni. Kwa maana ni jambo jema moyo kufanywa imara kwa neema; si kwa vyakula, ambavyo havijawafaa wale waliojishughulisha navyo.

.....

Kama ambavyo tumeweza kuisoma mistari hii,,tunamwona Mtume Paulo akiwa anawasilisha majaribu matatu muhimu ambayo yanasaidia kufunua kama mtu anaishi kama Mkristo wa kweli.

Jaribio la Kwanza kabisa ni kuhusiana na Upendo wa Kweli.

Katika aya ya kwanza,,Mtume anahimiza na kusema kuwa:“Upendo wa kindugu uendelee.”Hii bila shaka ni kuhusiana na jinsi ambavyo tunawatendea watu wengine.

Tukirejelea andiko kwenye Injili ya Yohana 13:35,,tunamwoona Bwana wetu Yesu Kristo akiwaambia wanafunzi wake ya kuwa:“Hivyo watu wote watajua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.”

Mpendwa unayeniskiza,,Mkristo wa kweli huuonyesha upendo wake kwa vitendo.

Swali ni,,Je, sisi kama Wakristo tunawapokea watu Wengine?

Waraka huu kwa Waebrania unatuhimiza ya kwamba tuisahau,, kuwakaribisha wageni.

Baba yetu wa imani Abrahamu alifanya hivyo alipowakaribisha wageni nyumbani kwake bila kujua kwamba alikuwa akiwakaribisha malaika wa Mungu.

Fundisho kuu hapa ni kwamba sisi kama Wakristo tunapaswa kuwa,, wakarimu,,,tuwasaidie wengine,,,tuwe watu wa kuwakaribisha wageni na zaidi mno tuwe tayari kushiriki nao tulicho nacho.

Nakuuliza hivi,,,Je, wewe ni mtu ambaye unawajali wale watu ambao wanateseka?

Biblia katika somo la leo kwenye aya ya 3,,inasema hivi; “Wakumbukeni waliofungwa kana kwamba mmefungwa pamoja nao.”

Hii ina maana kwamba tunapaswa kuwa na huruma kwa wale wanaopitia shida.

Ndugu pamoja na dadangu,,,leo hii kuna watu wengi ambao wanateseka kwa sababu ya magonjwa,,umaskini,,na hata kupitia kwenye dhiki mbalimbali.

Mkristo wa kweli anafaa kuwaombea, kuwafariji, na zaidi sana kujihusisha na mahitaji yao.

Upendo wa kweli haujijali tu, bali pia unayajali mahitaji ya wengine.

Jaribio la Pili ni kuhusiana na Kutosheka na Kile ambacho Menyezi Mungu Amekupa.

Katika aya ya tano Biblia inasema kuwa;“Mazungumzo yenu yasiwe na choyo; muwe radhi na vitu mlivyo navyo.”

Rafiki yangu,,,dunia hii inatufundisha kutafuta zaidi kila wakati, lakini Mungu anatufundisha kuridhika.

Kutosheka hakumaanishi kuyakosa malengo maishani. Maana yake ni kumshukuru Mungu kwa kile ulicho nacho huku ukiendelea kumtumaini kwa mahitaji ya kesho.

Kuna jambo hili kuhusiana na ndoa na ningependa kukuuliza swali hili ya kwamba,,Je, wewe pamoja nami,,,tunaiheshimu Ndoa?

Kwenye aya ya nne katika Waraka huu kwa Waebrania,,,Biblia inasema;

“Ndoa na iheshimiwe na watu wote.”

Mpendwa,,ni Mungu Mwenyewe ndiye mwaanzilishi wa ndoa.

Kwa hivyo Mkristo wa kweli anatakiwa kuwa mwaminifu kwa mwenzake ,kuiheshimu ndoa,kuepukana na uasherati na uzinzi na zaidi sana,, kuyaishi maisha ambayo ni masafi mbele za Mungu.

Sababu ya kuridhika mtu wangu,,, ni ahadi ya Mungu maana kwenye kitabu cha Kumbukumbu la Torati 31:8 ambayo imenukuliwa kwenye Waraka huu kwa Waebrania 13:5,,,Bwana anahaidi na kusema,,,“Sitakuacha wala sitakupungukia kamwe.”

Tunapojua kwamba Mungu yuko pamoja nasi, tunaweza kuishi bila ya kuwa na hofu kubwa kuhusu ya kesho.

Ndiyo maana neno katika aya ya 6 linasema:“Bwana ndiye msaidizi wangu, sitaogopa.”

Mkristo wa kweli humtegemea Mungu kuliko mali, fedha, au nguvu za wanadamu.

Jaribio la Tatu ambalo ni la mwisho kutokana na fundisho hili la leo ni kuhusiana na *Kusimama Imara Katika Imani.*

Tunapolisoma neno kutoka kwenye aya ya 8,,,tunaambiwa kuwa;“Yesu Kristo ni yeye yule jana na leo na hata milele.”

Dunia hubadilika kila siku, lakini Yesu habadiliki.

Mkristo wa kweli anapaswa kuwa na imani iliyoimarishwa ndani ya Kristo.

Ninalo swali hapa hapa ya kwamba,,,Je, wewe pamoja nami,,,tunaifuata Mifano ambayo ni Miema?

Rafiki yangu,,Waraka huu kwa Waebrania unatuhimiza kuwaangalia viongozi wa kiroho walio waaminifu na kuiga imani yao.

Tunapaswa kujifunza kutoka kwa watu wanaolipenda Neno la Mungu,,,wale wanayoyaishi maisha ya kuushuhudia wema wa Mungu na zaidi sana wale wanaotembea kwa uaminifu mbele Zake.

Neno kwenye aya ya 9 linatuonya hivi; “Msichukuliwe huku na huku na mafundisho mengine ya kigeni.”

Leo kuna mafundisho mengi yanayoweza kuwapotosha watu kutoka kwenye kweli ya Mungu.

Mpendwa,,njia za kipekee za kusalia kuwa salama ni kupitia kwa kuisoma Biblia,kuomba kila siku,,kushikamana na Yesu na pia kujengwa katika neema ya Mungu.

Mtu ambaye imani yake imejengwa juu ya Kristo hawezi kuyumbishwa kwa urahisi.

Kwa mhtasari wa kuhitimisha Waraka huu kwa Waebrania 13,,,bila shaka tunavipata vipimo vitatu vya kujichunguza:

Kwanza kabisa jiulize kwamba,,Je, ninawapenda wengine cha ukweli?

Pili ni kwamba,, Je, nimeridhika na kile ambacho Mungu amenipatia?

Tatu na mwisho ni Je, nimesimama imara katika imani yangu?

Mtu wangu,,,bila shaka,, haya ndiyo majaribu ambayo Mkristo wa kweli hupita.

Tunapomtegemea Bwana wetu Yesu Kristo kila siku, bila shaka Yeye hutupatia uwezo wa kupenda, kuridhika, na kusimama imara hata katikati ya changamoto za maisha.

Jichunguze leo mbele za Mungu. Kama kunapo mahali ambapo umekuwa mdhaifu, mwombe Bwana akusaidie. Mungu hajawaita Wakristo kuwa wakamilifu, lakini amewaita kuwa waaminifu na kuendelea kukua katika neema yake kila siku.

Katika 2 Wakorintho 13:5 neno linatuambia hivi; “Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe.”

Natumai ya kwamba umepata kitu kizuri kutokana na fundisho hili la leo;

Ombi.....

Uliye tukuka Juu ya vyote na tena Mfalme wa wafalme,,tunakushukuru kwa ajili ya fundisho hili leo kuhusiana mtihani kwa Wakristo. Kwa kweli tutalizingatia kupitia kwa usaidizi wa Roho wako Mtakatifu.

Ni kwa Yesu tumeomba.....Amen.....

Rafiki yangu,,hiki Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu. Kipindi cha matumaini kutoka Twr.Leo mada yetu imekuwa ni;Mtihan
kwa Wakristo.

Tumeutoa kwenye Waraka kwa Waebrania 13:1-9.

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo kusomea mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Anwani hiyo ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,u hapa wimbo,, nimevipiga vita hii ikiwa ni cover ya wimbo huo.....

WIMBO.....

Asante sana Pa Maabudu,,,kwa wimbo huo Nimevipiga Vita.Bila shaka ni wimbo wa kutia Moyo.

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA

KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2

Barua Pepe-barua@twr.co.ke

Kwenye Youtube ni @twr.co.ke

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara.....Kwaheri